*Nordic Journal of African Studies 22(4): 213–235 (2013)*

# Muundo wa Kimofo-Sintaksia wa Kitenzi (Kt) cha Kinandi kwa Mtazamo wa Kiunzi cha Kanuni Finyu (Kkf)

Hellen Chesang BARNO
*University of Eastern Africa-Baraton, Kenya*

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza muundo wa mofosintaksia wa Kikundi Kitenzi (KT) cha Kinandi katika viwango vya mofo-sintaksia na uliongozwa na Kiunzi cha Kanuni Finyu (KKF). Vipengele vya nadharia hii vilivyotumika ni uhakikishaji, uunganishaji, usogezaji na pia nadharia ya Eksibaa. Sentensi za Kinandi zilizalishwa na kuhakikishwa na wathibitishaji wazawa na wasemaji wa lugha ya Kinandi. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa kipatanishi kiima ni cha lazima na huchomozwa katika kielelezo tungo katika sehemu ya kiuamilifu ya Kipatanishi Kiima (KptK)[1]. KptK hutokea katika sehemu mbili kulingana na wakati husika; mwanzoni katika wakati uliopo (Wkpo) na baada ya mzizi (mzz) wa kitenzi katika wakati uliopita na wakati ujao (Wkjo). Kwa upande mwingine, kipatanishi yambwa (KptY) hutokea mwishoni mwa kitenzi. Aidha, kibainishi cha ukanushi (Kns) hubadilika kutegemea idadi na nafsi (Nfs). Kwa kuhitimisha, imebainika kwamba KT cha Kinandi kimeundwa na vipashio vya kimofosintaksia na kwamba vinaweza kuchomozwa kwenye vifundo amilifu.

## ABSTRACT

This study investigated morphosyntactic levels of verb phrase structure (VP) of Nandi language using Minimalist Program (MP). The components of MP that were used included: feature checking, merge, move and also X-bar theory. Nandi sentences were generated and verified by native speakers of the Nandi language. The findings of this study show that the agreement subject (AgrS) can be projected in the functional nodes of the agreement subject 1 ($AgrS^1$) while the agreement object (AgrO) can be projected in the functional nodes of the agreement object 1 ($AgrO^1$). AgrS comes before the root of the verb in present tenses and after the root in the past and future tenses. The negative elements in a verb change depending on number and person. In conclusion, Nandi verb has morphosyntactic features which can be projected in the functional nodes in the VP structure.

***Maneno muhimu**: Kinandi, Kikundi Kitenzi, Kanuni Finyu, Mofosintaksia.*

# 1. UTANGULIZI

Kazi hii inatokana na uchanganuzi wa mofo-sintaksia ya Kikundi kitenzi cha Kinandi. Kinandi ni lugha mojawapo ya lugha zinazozungumzwa katika nyanda za juu Magharibi mwa Kenya (Hollis, 1909; Creider, 2002). Ninapendekeza kwamba lugha hii ina vipashio vya kimofosintaksia kadhaa vikiwemo: wakati, hali, ukanushi, uyakinishi, kipatanishi yambwa na kipatanishi kiima. Vipashio hivi huwa vimeambikwa katika kitenzi na huathiri muundo wa kirai au sentensi katika kiwango cha kiuamilifu tukizingatia nadharia ya KF. Kwa mantiki hii nimeshughulikia mofosintaksia kwa kuhusisha Nadharia ya Kanuni Finyu ya Chomsky 1995 na 2000.

Nadharia hii ya Chomsky ni mojawapo ya nadharia ambazo zimekuwa zikibadilika kadri wakati unavyozidi kusonga ili kusahilisha na kuweka wazi uchambuzi wa lugha. Utafiti huu ulitumia vipengele vya nadharia hii kama: Uhakikishaji, Uunganishaji na Usogezaji na pia nadharia ya Eksibaa.

Data iliyotumika ilikusanywa kutokana na wasemaji wazawa wa Kinandi walioteuliwa kimakusudi. Aidha, mtafiti akiwa msemaji mzawa wa Kinandi alitumia umilisi wake wa lugha husika katika kuainisha na kuchambua data.

# 2. MUUNDO WA KIMOFOSINTAKSIA YA KIKUNDI KITENZI CHA´ KINANDI

Mofosintaksia ni vipashio vya kimofolojia ambavyo uamilifu wake hubainika katika sintaksia kama vile, njeo, hali, ukanushi (n.k.). Kwa mfano, kitenzi cha kinandi *kikipir* kina sifa za mofolojia:

| | |
|---|---|
| *ki*- | kiambishi cha wakati |
| -*ki*- | nafsi ya tatu |
| -*pir*- | mzizi wa kitenzi |

Kisintaksia, {ki-} na {ki-} mtawalia husimamia kiwakilishi wakati na kipatanishi kiima:

| | |
|---|---|
| *ki*- | kiwakilishi cha wakati |
| -*ki*- | kipatanishi kiima |
| -*pir*- | mzizi wa kitenzi |

Kwa sababu maneno huwa yameambikwa tayari katika sintaksia, mofu hizi zitawakilishwa katika vifundo vya kiuamilifu ambavyo ni: Kiwakilishi wakati (Wkt[1]), Kiwakilishi Kipatanishi Kiima (KkptK[1]), Kiwakilishi Kipatanishi Yambwa, Ukanushi, Hali n.k., kama itakavyoonyeshwa katika vielelezo tungo vitakavyofuata. Vipashio hivi huathiri ufasiri wa sentensi. Taaitta Toweett (1979) akishughulikia isimu ya Kikalenjin anaonyesha viambishi mbalimbali vinavyoambikwa kwenye vitenzi na ambavyo hubeba sifa za kimofosintaksia.

Katika Kinandi, kitenzi hubeba viambishi vya nafsi, wakati, hali na ukanushi. Creider (2002) anahoji kwamba vitenzi vya Kinandi vinaambikwa viambishi vya yambwa, kiima, dhamira, njeo, hali na ukanushi. Hata hivyo, mfumo wa viambishi vya vitenzi vya Kinandi hauchukui viambishi vingi kwa wakati moja; vitenzi tofauti huonyesha sifa hizi kwa nyakati tofauti. Kwa mfano:

(1) *Tien-i* - Anaimba
Mzz-Wkpo- $H_{kuendelea}$

(2) *Ki – tien-i* - Alikuwa akiimba
Wkpt1-Mzz- $H_{kuendelea}$

(3) *Ki- i –tien* - Uliimba
Wkpt-Nfs2-Mzz

(4) *Tun a-tien-i* - nitaimba
Wkjo-Nfs1-Mzz-$H_{kuendelea}$

Kulingana na paradimu hii, kitenzi cha wakati uliopo (Wkpo) cha Kinandi hakina kibainishi wazi cha wakati, kwani, mtu anaposema *atieni*, inaeleweka kuwa anaimba wakati huu. Katika mfano (1) na (2) kibainishi kiima pia si wazi kama ilivyo katika mifano (3) na (4). Mofu {-i} inasimamia hali ya kuendelea na hutokea baada ya mzizi wa kitenzi katika mifano (1), (2) na (4). Kibainishi cha wakati, uwe wakati uliopita ama wakati ujao, huja kabla ya kipatanishi kiima. Kwa mfano {ki-} ni kibainishi cha wakati uliopita (Wkpt1) na wakati uliopita huwa na vibainishi vitatu: {ki-} kikiwa cha kwanza {ko-} kikiwa cha pili na {ka-} kikiwa cha tatu kama ilivyoelezewa katika mfano (5) hapo chini. Kipatanishi kiima katika lugha ya Kinandi huja baada ya wakati. Kwa mfano {-a-} na {-i-} kulingana na mifano iliyopo katika paradimu hapo chini.

Kipatanishi kiima huja kabla ya mzizi wa kitenzi na kinaweza kuwa katika nafsi ya kwanza na ya pili. Kwa upande mwingine mofu ya kipatanishi kiima hutokea mwishoni mwa kitenzi katika nafsi ya tatu wingi na ni kapa katika nafsi ya tatu umoja. Aidha, kipatanishi kiima huchukua sifa ya idadi kwa sababu kinaweza kuwa katika umoja au wingi (5):

| | | | |
|---|---|---|---|
| (5) | a. | Umoja | Wingi |
| | | *Ka-i-tien* | *ka-o-tien* |
| | | Wkpt3-Nfs2U-mzz | Wkpt3-Nfs2W-mzz |
| | | Uliimba | mliimba |
| | b. | ko-a-tien | ko-ke-tien |
| | | Wkpt2-Nfs1U Mzz | Wkpt2-Nfs1W-Mzz |
| | | Niliimba | tuliimba |

| | | |
|---|---|---|
| c. | ki-*ko-tien* | *ki-ko-tien-sho* |
| | Wkpt1-$H_{timilifu}$-Mzz | Wkpt- $H_{timilifu}$-Mzz-Nfs3W |
| | ameimba | Wameimba |
| d. | *Ka-tien-i* | *ka-tien-ndos* |
| | Wkpt3-Mzz-Nfs3U-$H_{kuendlea}$ | Wkpt3-Mzz-Nfs3W |
| | Alikuwa anaimba | walikuwa wanaimba |

Katika mfano (5a) ni kuwa, kibainishi cha nafsi ya pili umoja kinatokea baada ya wakati uliopita kabla ya kitenzi. Mofu {-i} katika mfano (5a) hapo juu, inasimamia nafsi ya pili umoja na mofu {-o} inasimamia nafsi ya pili wingi. Katika mfano (5b), mofu {-a} inasimamia nafsi ya kwanza umoja na mofu {-ke) nafsi ya kwanza wingi. Katika mfano (5c) na (5d) mofu ya nafsi ya tatu umoja ni kapa; na hivyo, si dhahiri. Kwa upande mwingine mofu inayosimamia wingi katika nafsi ya tatu wingi ni {-sho} katika (5c) na {-ndos} katika (5d) na ambayo hutokea mwishoni mwa kitenzi. Kipatanishi Yambwa kwa upande mwingine hutokea mwishoni mwa kitenzi (6):

| | | |
|---|---|---|
| (6) | Ka-i-tien-chi | ka-o-tien-chi |
| | Wkpt-KptK-Mzz-KptY | Wkpt-KptK-Mzz-KptY |
| | Umemwimbia | mmemwimbia |

## 3. NJEO KATIKA KINANDI

Njeo ni kategoria ya kimofosintaksia ambayo huwakilisha uhusiano kati ya wakati wa tendo na wakati wa urejelezi ama wakati wa mazungumzo. Pia, inaweza kuwa uhusiano wa mada na wakati wa matamshi. Pia, njeo ni kiunganishi cha tukio na ni kategoria amilifu ya kisintaksia. Katika lugha nyingi njeo ina dhima muhimu ya kutofautisha nyakati kisemantiki (Osawa, 1999). Madai haya yanashabihiana na dhima ya njeo katika lugha ya Kinandi. Hii ni kwa sababu njeo ni kibainishi kionyeshi cha wakati. Katika Kinandi, kuna nyakati mbalimbali: wakati uliopita, uliopo na ujao.

Kwa mfano:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (7) | Kinandi | | Wakati | | Kiswahili |
| | *Atieni* | - | wakati uliopo | - | Ninaimba |
| | *Katieni* | - | wakati uliopita | - | nilikuwa ninaimba |
| | *Tunatieni* | - | wakati ujao | - | nitaimba |

Chomsky (1995) anabainisha sifa zinazofasirika na zile zisizofasirika. Sifa zinazofasirika zina maana ya kisemantiki na zinatumiwa kufasiri kipashio/mofu katika sentensi. Sifa hizo husalia baada ya mchakato nyanyuzi hadi katika umbo la kimantiki (UMM). Sifa zisizofasirika katika kitenzi hazina maana

kisemantiki. Idadi na nafsi hunyanyuliwa hadi kwenye KptK[1] kwa sababu kina sifa ya kipatanishi kiima. Kwa upande mwingine, sifa za upatanishi katika kipatanishi yambwa hunyanyuliwa hadi kwenye nafasi ya KptY[1] ili kuhakikisha sifa za upatanishi na nyakati. Kitenzi hunyanyua sifa zake hadi kwenye vipatanishi, nyakati na hali katika umbo la kimantiki. Katika vielelezo tungo vilivyochorwa hapo chini, sifa amilifu katika kitenzi ambazo zimenyanyuliwa kwa ajili ya kuhakikishwa vimeonyeshwa. Nadharia ya uhakikishaji imeibuka na vifundo vya kiuamilifu katika mchakato wa ujenzi wa muundo. Kwa mfano, kifundo cha kptK[1] katika vielelezo tungo vinahakikisha uhusika. Kifundo cha wkt[1] kimezalishwa kuhakikisha njeo na kifundo cha hali (hl) ya kuendelea, mazoea ama timilifu kimezalishwa ili kuhakikisha hali husika. Kulingana na Kanuni Finyu, uhakikishaji ni njia ya kuthibiti usarufi wa tungo.


Palmer (1986) anaonyesha kuwa uhusiano wa njeo na wakati si wa moja kwa moja. Inasemekana kuwa njeo ni usarufishaji wa wakati, ama ni mfumo wa kimuktadha ambao unahusisha wakati wa tendo na wakati wa usemaji (Lyons, 1995). Hivyo, kuna tofauti kati ya wakati uliopita na wakati uliopo na tofauti hizi huonyesha tofauti ya kitenzi kimoja na kingine;

(8) *Wendi Cherotichstashon* - Cherotichanaendastasheni
Wkpo Km Mhl

Katika Kinandi, kuna nyakati mbalimbali ambazo huwakilishwa na viambishi mbalimbali. Wakati uliopita huchanganuliwa kwa kuzingatia ufupi au urefu wa muda ambapo tendo lilifanyika. Kuna wakati uliopita wa muda mrefu sana, muda mrefu kiasi na muda mfupi sana. Wakati uliopita wa muda mrefu huonyeshwa kwa kibainishi {ki-} ilhali wakati uliopita ambao ni wa muda mrefu kiasi huonyeshwa kwa kibainishi {ko-} na wakati uliopita wa muda mfupi sana huonyeshwa kwa kibainishi {ka-}. Pia kuna kibainishi {kitun-} cha kinathari cha wakati uliopita ambacho mara nyingi hutumika katika masimulizi. Kibainishi hiki kinajumuisha kibainishi cha wakati uliopita wa mbali {ki-} na ya wakati ujao {tun-}. Kibainishi hiki ni changamano kwa sababu viambishi vya wakati mbili hutokea kwa wakati mmoja. Kibainishi hiki pia hutokea pamoja na kibainishi cha hali timilifu. Kwa mfano:

(9) Ki-tun-ko-ki-mii (palikuwepo)
Wkpt1-Wkjo-$H_{timilifu}$-KptK-Mzz
Vibainishi vya wakati katika Kinandi ni kama vifuatavyo:

[ki-] - muda mrefu
[ko-] - muda mrefu kiasi
[ka-] - muda mfupi
[kitun] - muda mrefu sana wa nathari - kiambishi hiki hakitashughulikiwa katika utafiti huu ila kutajwa tu.




Mifano:

(10) *Ki-i -but missing* (alianguka sana)
Wkpt1-KptK-Mzz E

(11) *Ko-i-but* (alianguka)
Wkpt2-KptK-Mzz
Kitenzi hiki *koibut* katika (11) kina maana kwamba kuanguka huku kulitokea si kitambo sana bali kulitokea labda saa chache tu kabla ya matamshi.

(12) *Ka-i-but (*alianguka)
Wkpt-KptK-Mzz

Maana ya kitenzi *kaibut* ni kwamba kilichoanguka kilianguka dakika chache kabla ya matamshi.

(13) $^{*}$*Ki-tun ko-ki-i-but* (alianguka kitambo)
Wkpt-Wkjo-$\text{H}_{\text{timilifu-}}$Wkpt-KptK-Nfs3-Mzz

Maelezo ya kitenzi hiki ni kwamba kuanguka huku kulitokea miaka mingi sana iliyopita ambayo labda haiwezi kuhesabika au kukadirika.

## 4. WAKATI ULIOPITA MUDA MREFU SANA


Katika Kinandi kibainishi cha wakati uliopita muda mrefu sana ni {ki}. Kibainishi hiki kinaonyesha kwamba tendo lilitendeka miaka kadhaa iliyopita. Kibainishi hiki kinaingiliana na hali timilifu ya tendo. Yaani, tendo lililotendwa miaka mingi iliyopita lilikamilika. Kwa mfano:

(14) *Ki-ki*-bar (aliuawa)
Wkpt1-KptK-Mzz

(15) *Ko-ki-bar (*aliuawa)
Wkpt2-KptK-Mzz

(16) Ka-ki-bar (aliuawa)
Wupt3-KptK-Mzz

Vielelezotungo vitakavyofuata vimetumiwa kuonyesha jinsi vipashio vya kimofo-sintaksia vinavyonyanyuliwa ili kuhakikisha sifa zao za njeo, upatanifu, hali na ukanushi. Kwa mfano:




**Kielelezo 1**. *Tungo*

Katika kielelezo 1 viambishi ambavyo vimechopekwa kwenye kitenzi vimenyanyuliwa ili kuhakikisha sifa zake katika sehemu husika. Kibainishi cha wakati {ko-} kimenyanyuliwa hadi kwenye Wkt$^1$ ili kuhakikisha sifa za nyakati. Kwa upande mwingine kibainishi cha kiima {ki-} kimenyanyuliwa hadi kwenye KptK$^1$ ili kuhakikisha sifa za idadi na nafsi. Katika vielelezo vitakavyofuata uhakikishaji huu utafanyika, hivyo, maelezo haya yatashughulikia vielelezo vingine.

Sehemu ambapo kionyeshi cha wakati uliopita wa muda mrefu sana kimekaa ndipo vionyeshi vya wakati uliopita muda mrefu kiasi na wakati uliopita wa muda mfupi sana vitawekwa katika kielelezo tungo. Kama ilivyoonyeshwa katika vielelezo tungo, katika Kinandi, kipatanishi kiima hutokea baada ya kibainishi cha wakati. Kwa mfano, katika (17) kibainishi {ko-} cha wakati kimetokea kabla ya kibainishi {ki-} cha kiima.

(17) *Ko-ki-bar* (aliuawa)
Wkpt2-kptK-Mzz

## 5. WAKATI ULIOPITA WA MUDA MREFU KIASI

Wakati uliopita ambao si wa muda mrefu sana hutumia kibainishi {ko-} ambapo kionyeshi hiki kinabainisha kuwa tendo lilitendeka miezi michache iliyopita, wiki moja iliyopita, siku au saa chache zilizopita.

(18) *Ko-ki-pir* (alipigwa)
Wkpt2- KptK-Mzz

Kibainishi cha nafsi na idadi {ki-} katika kitenzi kilicho (18) hapo juu kinaweza kuwa nafsi ya tatu umoja ama nafsi ya tatu wingi. Kisemantiki {ki-} ni mofu tata kwa sababu kina sifa ya umoja ama wingi, kisintaksia ni kipatanishi kiima na maana yake itategemea kipatanishi kiima kinachofuata ama kiwe kwa umoja au kwa wingi. Kwa mfano:

(19) *Ko-ki-pir-o anee* (nilipigwa)
Wkpt2-kpK-Mzz-kptY mimi

(20) *Ko-ki-pir-ech achek* (tulipigwa)
Wkpt2-kptK-Mzz-kptY sisi

(21) *Ko-ki-pir-in inyee* (ulipigwa)
Wkpt2-kptK-Mzz-kptY wewe

(22) *Ko-ki-pir-ok okwek (*mlipigwa )
Wkpt2-kptK-Mzz-kptY nyinyi

(23) *Ko-ki-pir inee*(alipigwa)
Wkpt2-kptK-Mzz yeye


(24) *Ko-ki-pir ichek* (walipigwa)
Wkpt2-kptK-Mzz wao

(25) **Ko-ki-pir anee** (alipigwa mimi)

(26) **ko-ki-pir-inyee**(alipigwa wewe)

Kibainishi kipatanishi kiima cha Kinandi {ki-} kama ilivyo katika 19-26 hutokea katika nafsi zote tatu. Kinachotofautisha nafsi hizi zote tatu katika sentensi ni: idadi kwa mfano *anee*

(mimi) nafsi ya kwanza umoja, *achek* (sisi) nafsi ya kwanza wingi, *inyee* (wewe) nafsi ya pili umoja, *okwek* (nyinyi) nafsi ya pili wingi, *inee* (yeye) nafsi ya tatu umoja na *ichek* (wao) ikiwa ni nafsi ya tatu wingi. Mofu zinazobainisha vipatanishi yambwa katika nafsi mbili, isipokuwa nafsi ya tatu ambayo haina vipatanishi yambwa ni: (-o) katika nafsi ya kwanza umoja, (-ech) katika nafsi ya kwanza wingi, (-in) katika nafsi ya pili umoja na (-ko) katika nafsi ya pili wingi. Vibainishi hivi vyote hutokea baada ya mzizi wa kitenzi:





**Kielelezo 2**.

## 6. WAKATI ULIOPITA WA MUDA MFUPI

Wakati wa aina hii hubainishwa kwa kibainishi {ka-} ambacho hurejelea wakati wa matamshi ambao si wa muda mrefu. Tendo linaweza kuwa limefanyika dakika chache tu kabla ya matamshi. Kwa mfano:

(27) *Ka-i-twal* (aliruka)
Wkpt3- KptK-Mzz





**Kielelezo 3**.

## 7. WAKATI ULIOPO

Wakati uliopo katika Kinandi hauna kibainishi wazi cha wakati bali tendo hutokea sambamba na wakati. Mara nyingi huongezewa vivumishi vya wakati ama lieleweke tu jinsi lilivyo. Katika Kinandi, mtu anaposema *awendi*, linatosha kuwa anaenda sasa hivi. Hivyo, mzungumzaji anapotamka tendo huwa linatendeka. Ama msemaji anaweza kuongezea vivumishi vya wakati. Kwa mfano:

(28) *A-wendi nguno* (ninaenda sasa hivi)
KptK-Mzz- Vwt




**Kielelezo 4**.

Katika hali hii, kipatanishi kiima hutokea mwanzoni mwa kitenzi. Mofu (a-) ndiyo inayochukua nafasi ya nafsi ya kwanza umoja na kipatanishi kiima. Kisemantiki, mofu hiyo hiyo inachukua nafasi ya idadi na nafsi. Katika hali hii, mofu {a-} inachukua idadi ya umoja na nafsi ya kwanza. Katika mfano (28) kibainishi cha wakati kimedondolewa na hivyo si wazi.


## 8. WAKATI UJAO WA KARIBU

Wakati ujao unaweza kuwa wa muda mrefu au mfupi. Kibainishi cha wakati ujao wa muda mfupi si wazi lakini kibainishi cha wakati ujao wa muda mrefu ni {tun-} ili kuonyesha kuwa tendo litatendeka baada ya wakati fulani baada ya matamshi. Katika wakati ujao wa muda mfupi, mtu anaweza kusema tu jinsi ilivyo ama atumie vivumishi vya wakati. Wakati ujao ambao ni wa muda mfupi hufanana na wakati uliopo ambao hauna vibainishi wazi katika Kinandi. Kwa mfano:

(29) *Nyon-e-i* (anakuja)
Mzz-kptK-$H_{kuendelea}$

(30) *Nyon-e-i nguno* (atakuja sasa hivi)
Mzz-kptK-$H_{kuendelea}$ Vwt

(31) *Nyon-e-i sait loo* (atakuja saa sita)
Mzz-kptK-$H_{kuendelea}$ Vwt





**Kielelezo 5**.

Kitenzi *nyonei* (30) kisemantiki kina maana kwamba anayekuja atakuja wakati wowote kuanzia sasa, lakini anaweza kuchukua muda mrefu au muda mfupi. *Nyonei saa ii* (30) ina maana kwamba anayekuja atakuja sasa hivi wala hatakawia. Kwa upande mwingine, *nyonei sait loo* (31) ina maana kwamba wakati wa kuja kwake ni dhahiri na kibainishi chake ni wakati wenyewe ambao ni saa sita.

## 9. WAKATI UJAO WA MUDA MREFU

Wakati ujao una maana kuwa tendo litachukua muda mfupi au mrefu ili litendeke baada ya matamshi. Kwa mfano:

(32) *Tun-nyon-e-i* (atakuja)
Wkjo-Mzz-KptK-IT




**Kielelezo 6**.

## 10. HALI

Kulingana na Comrie (1976), hali ni mtazamo wa vipashio vya ndani vya wakati na jinsi tendo linavyofanyika. Hivyo, hali inatupa njia tofauti ya kuchanganua vipashio vya ndani vya tendo. Kwa mfano swali litakaloulizwa ni kwamba, tendo lilitendeka wakati gani? lilifanyikaje? na je, tendo limekamilika au bado

linaendelea? Isitoshe, Comrie (1976) anatoa tofauti kati ya njeo na hali. Anasema kwamba njeo huhusu wakati wa hali inayorejelewa na kwa upande mwingine, hali ni jinsi tofauti ya kuelezea vipashio vya ndani vya wakati. Kulingana na kijelezi hiki ni kana kwamba hali ni kivumishi cha wakati. Hii ni kwa sababu baada ya wakati kufanya kazi hali inaelezea zaidi jinsi tendo hilo lilivyofanyika. Je? tendo lilikamilika au linaendelea. Kwa upande mwingine, je? Tendo hilo lilitendeka kwa kasi au polepole. Hivyo, hali inaelezea jinsi tendo lilifanyika katika wakati fulani. Kijelezi hiki kinaingiana na muundo wa hali katika Kinandi kwa sababu hali huelezea zaidi jinsi tendo lilifanyika.

(33) [Njeo[Hali[Maelezo ya matukio]]]

Inasemekana kwamba utendakazi wa hali unafasiriwa kama vivumishi, hivyo, unaonyesha seti ya matukio katika aina nyingine ya matukio. Njeo huonyesha matukio katika wakati kwa kurejelea mahali na wakati wa matukio. Hivyo, kulingana na madai haya njeo huvumishwa na wakati na ina sifa za kimofosintaksia.

Katika Kinandi, vitenzi mbalimbali hudokeza hali ya aina mbalimbali, kwa mfano: hali ya kukamilika kwa tendo, hali ya kuendelea ama jinsi kitenzi kinavyofanya tendo ama kwa haraka au polepole. Kuna dai kuwa kategoria ya hali hubainishwa katika kiwango cha muundo wa kiarifu-kishiriki, na ambayo hutambuliwa kama maelezo ya matukio. Dhima ya hali katika Kinandi kama ilivyo katika lugha nyingi ni kuelezea zaidi kuhusu jinsi tendo limefanyika. Hivyo, hali ni kama kivumishi cha wakati ambapo tendo lilifanyika. Je, tendo limefanyika? kwa mfano, *kakwo* (ameenda) ama linaendelea kufanyika? *Wendi (*anaenda).

## 11. VITENZI VYA HALI HALISI KATIKA KINANDI


Kuna vitenzi vinavyoonyesha hali tofauti tofauti za vitenzi vya Kinandi. Kuna vitenzi vinavyoonyesha hali ya kitenzi ambacho hakiwezi kugawanywa, vitenzi vinavyofanya kazi katika muda mfupi (n.k.) Givon' (2001) amegawa vitenzi katika viwango vikuu kwa kutegemea hali yao ya asili: Kwanza, kitenzi cha hali iliyounganishwa, na pili, kitenzi cha muda mfupi. Vitenzi vilivyoorodheshwa hapa chini vinachukua sifa za vitenzi vya muda mfupi katika Kinandi.

(34) a. {-*bet-*} - pasua
Mzz

b. {-*mwook-*} - piga bunduki
Mzz

c. {-*twal-*} - ruka
KptK-mzz

d. {-*kwer-*} - gonga
Mzz




**Kielelezo 7**.

Vitenzi vya aina hii vinaonyesha kuwa hali ya kufanya tendo hili ni kwa haraka. Vitenzi vya aina hii hutokea pamoja na mofu ya wakati uliopita ama katika kauli ya kuamuru. Kulingana na mfano (1.7) ni kwamba tendo lilifanyika kwa haraka na limekamilika. Sehemu ambapo kitenzi *kimwook* kimekalia katika kielelezo tungo ndipo mahali ambapo vitenzi, *bet, twal* na *kwer* vitakalia.

## 12. VITENZI VYA HALI TIMILIFU

Vitenzi vya hali timilifu katika Kinandi vinaonyesha kuwa tendo lililotendwa limekamilika. Vitenzi vya aina hii vinaweza kutiwa mofu ya hali timilifu {–ko} au {-ke}. Hali timilifu hutokezea na mofu za wakati uliopita, kwa mfano; {ki-}, {ko-}, {ka-}. Vitenzi vya hali timilifu havina viambishi tamati. Hivyo, vitenzi hivi huishia kwa mzizi wa kitenzi. Kwa mfano:


(35) a. *Ka-ko-it* - amefika
Wkpt3.KptK-Ht-Mzz

b. *Ki-ko-nyor* - amepata
Wkpt1.KptK-Ht-Mzz

c. *Ka-ko-mee* - amekufa
Wkpt3.KptK-Ht-Mzz

d. ka-*ke-sich* - amezaliwa
Wkpt.KptK-Ht-Mzz

e. *ko-ko-tar* - amemaliza
Wkpt2.KptK-Ht-Mzz




**Kielelezo 8**.

## 13. VITENZI VYA HALI YA UTENDAJI AU YA KUENDELEA

Vitenzi vya hali ya utendaji vina sifa ya hali ya kuendelea. Mofu zinazoonyesha hali hii si bainifu kwa sababu vitenzi vyenyewe vinaonyesha kuwa tendo linaendelea kufanyika. Vitenzi hivi hutokea kuwili, vile ambavyo vinadhihirishwa na mofu ya wakati wa kuendelea ambayo ni mofu {-i} na vile ambavyo vitenzi vyenyewe vinasimamia wakati uliopo. Vitenzi hivi vyote huwa vinaishia na kiishio {- i}. Hali ya kuendelea hutokea sambamba na wakati uliopo na wala si pamoja na wakati uliopita. Kwa mfano:

(36) a. *Tu-e-i* - anapasua
Mzz- KptK-$H_{endelea}$

b. *I-guiguch-i* - anakunywa
KptK-Mzz-$H_{kuendelea}$

c. *Tiech-e-i* - anakanyaga
Mzz-KptK-$H_{kuendelea}$

d. *Wend-a- ti* - anatembea
Mzz-KptK-$H_{kuendelea}$

e. *Som-a-ni* - anasoma
Mzz-KptK-$H_{Kuendelea}$

Vitenzi vya hali/jinsi katika Kinandi huonyesha hali ilivyo wakati wa matamshi. Mofu inayotangulia vitenzi hivi ni (ke-) ambayo inalingana na kitenzi kisaidizi *kuwa* katika Kiswahili na *to* katika lugha ya Kiingereza. Mifano ya aina ya vitenzi hivi katika lugha ya Kinandi ni:

(37) a. *Ke-arogen* - kuwa na wasiwasi
Kw-Mzz

b. *Ke-kaititit* - kuwa baridi
Kw-Mzz

c. *Ke-nai* - kujua
Kw-mzz

d. *Ke-mach* - kutaka
Kw-mzz


e. *Ke-goit* - kuwa refu
Kw-Mzz

f. *Ke-biririt* - kuwa nyekundu
Kw-mzz

Aina ya vitenzi tulivyoorodhesha hapo juu vitatusaidia kugawa hivi vitenzi katika hali timilifu na hali isotimilifu. Katika sehemu inayofuata, tumechambua hali timilifu na isotimilifu katika Kinandi na jinsi hali inavyoweza kuchomozwa katika vielelezo tungo.

## 14. HALI TIMILIFU NA ISOTIMILIFU

Katika Kinandi, utimilifu unahusu wakati ambao una mpaka wa muda, hali inaweza kuwa wakati wenye mpaka na pia inaweza kuwa muda mrefu au mfupi. Kuna dhana mbili zinazohusiana na hali katika lugha hii, nazo ni hali timilifu na hali isotimilifu. Hali hizi zinaweza kuelezwa kwa njia ifuatayo.





Hali timilifu inahusu ukamilikaji na mpaka wa tendo linalohusiana na wakati uliopita. Uunganishwaji wa kitenzi hutokea katika hali timilifu na hufasiriwa kama tukio.

Vitenzi vya hali hutokea katika hali isotimilifu. Hali isotimilifu inaweza kuwa hali inayoendelea ama isokikomo na ambayo huelezea hali inayoendelea kwa kurejelea wakati. Vitenzi hivi vinatumika na viarifu vyenye kubadilika bali si vitenzi vya jinsi/hali. Hali ya kuendelea katika muktadha huu imebainishwa na mofu {-she-} na kwa upande mwingine, wakati uliopo umebainishwa na mofu {-i} katika (38).


Kwa mfano:

(38) *I-bat-i-she-i* (analima)
KptK-Mzz-Wkpo-$H_{endelea}$-IT




**Kielelezo 9**.

Katika Kinandi, hali ya kuendelea hutokea katika nyakati zote tatu. Mofu inayoashiria hali ya kuendelea katika wakati ujao ni {-she-}, hivyo, kielezo tungo kitakuwa kama ilivyo hapo chini. Kitakachobadilika ni kibainishi cha wakati. Kwa mfano *ibatishei* ina maana kuwa anayelima analima wakati msemaji anapotamka na kwa upande mwingine (38 b) *kaibatishei (*alikuwa akilima) ina maana kwamba wakati msemaji alipotoka pale kitendo cha kulima kilikuwa kikiendelea.





**Kielelezo 10**.

Katika Kinandi, hali isotimilifu inaweza kuwa hali ya kuendelea ama hali ya kurudiarudia tendo fulani. Hali hii huonyesha kuwa tendo linaendelea kufanyika na kuwa halijakamilika. Hali isotimilifu inaweza kuwa inayoendelea au isokikomo, ama ambayo huelezea vitendo vinavyoendelea na hali ya mazoea ambayo inaelezea matukio yanayorudiwa (Givon, 2001). Hali ya mazoea huelezea matendo yanayofanyika kila mara ama yanayojirudia. Matukio haya huwekwa katika kategoria ya hali wala si njeo (Dahl, 1985). Kibainishi cha hali hii katika Kinandi ni (cham-) na hali hii hutokea katika wakati uliopo pamoja na wakati uliopita. Mofu inayotokea na mofu ya hali ya mazoea {-cham-} ni {ki-} ambayo ni ya wakati uliopita huku ikionyesha kwamba tendo lilikuwa likifanyika kila mara lakini limekamilika ama tendo bado linaendelea. Vitenzi hivi vya hali ya mazoea huwa vimeambikwa mwanzo na mwisho. Kwa mfano:

(39) a. *Cham-ko-tien-i* (huwa anaimba)
$H_{mazoea-}$ KptK-Mzz-$H_{kuendelea}$

b. *Cham-ko-labat*-i (huwa anakimbia)
$H_{mazoea}$-KptK-Mzz-$H_{kuendelea}$


c. *Ki-cham-ko-labati*- (alikuwa akikimbia)
Wkpt-$H_{mazoea}$-KptK-Mzz-$H_{kuendelea}$




**Kielelezo 11**.


Katika Kinandi kibainishi cha kuonyesha kuwa fulani huimba au anakimbia katika hali ya kuendelea hutokea katika wakati uliopo pamoja na wakati uliopita. Katika wakati uliopo kitenzi huambikwa katika sehemu ya mwanzo wa mofu {i-} ambayo hutokea mwishoni mwa kitenzi. Katika hali ya mazoea, kitenzi huwa na mofu ya hali ya mazoea {cham-} na mofu ya wakati uliopita {ki-} kwa maana kuwa tendo lilikuwa linatendeka kila mara lakini limekamilika. Pia, hali ya kuendelea inaweza kuongezewa vivumishi vya nyakati, kwa mfano, *tienikotugul* kumaanisha kuwa fulani huwa anaimba kila mara. Aidha, hali hii huweza kuonyeshwa katika matumizi ya uradidi wa vitenzi; kwa mfano, *tienatieni* (huimbaimba), *labatati* (hukimbiakimbia).

(40) *Tien-i kotugul* (huimba kila mara)
Mzz-IT Vwk




**Kielelezo 12**.

(41) *Tien-a-tien-i* (anaimbaimba)
Mzz-KptK-Mzz-IT




**Kielelezo 13**.

Pia hali isotimilifu ama ya kuendelea katika Kinandi hutokea sawasawa na wakati uliopo. Hii ni kwa sababu mnenaji anapotamka *tieni* (anaimba) ina maana kwamba anayeimba anaendelea kuimba ama tendo la kuimba linaendelea:


(42) a. *Tieni* (naimba)

b. *Wendi* (anaenda)


c. *saei* (anaomba)

*d.* *maei* (anaanika)

Usambamba wa wakati uliopo na hali ya kuendelea hutokana na ukweli, kwamba katika dhana zote hudokeza kuwa tendo linafanyika sasa na katika hali ya kuendelea wala si katika hali ya kukamilika. Kama ilivyo katika wakati uliopo, vibainishi vya hali ya kuendelea si dhahiri bali kitenzi hueleweka tu jinsi kilivyo. Kwa mfano, *saei* katika Kinandi linaeleweka kuwa fulani anaendelea kuomba.




**Kielelezo 14**.




**Kielelezo 15**.

Vitenzi *saei* na *wendi* vinadokeza kwamba vitendo vinaendelea kutendeka wakati wa matamshi.

## 15. HALI TIMILIFU

Hali timilifu katika lugha nyingi huwa na wakati uliopita ilhali hali isotimilifu inaweza kutumika na wakati ujao (Dahl, 1985). Anaelezea kuwa kibainishi cha wakati timilifu kwa mfano *me* katika lugha ya Kiswahili hufanya kazi ya njeo na hali. Vibainishi vinavyotumika kuashiria hali timilifu katika Kinandi ni vitatu; {ko-}, {ke-} na {ki-} ambavyo vinatumika katika wakati uliopita:

(43) a. *Ka-ko-tien* (ameimba)
Wkpt3-$H_{timilifu.}$kptK-Mzz

b. *Ko-ko-tien* (aliimba)
Wkpt2-$H_{timilifu.}$kptK-Mzz

c. *Ki-ko-tien* (aliimba)
Wkpt1-$H_{timilifu.KptK}$-Mzz


d. *Ki-kwo* (ameenda)
Wkpt.$H_{timilifu}$-mzz

e. *Ki-ka-kwo (*alikuwa ameenda)
KptK-Wkpt.$H_{timilifu-}$Mzz

f. *Ka-a-tien* (nimeimba)
Wkpt-KptK-Mzz

g *A-tien-i* (Ninaimba)
KptK-Mzz-$H_{kuendelea}$

h. *Ka-ke-tien* (Tumeimba)
Wkpt-KptK-Mzz




**Kielelezo 16**.


## 16. UKANUSHI

Ukanushi ni hali ya kukana tendo. Mofu za ukanushi ni mofu ambazo huwekwa katika vitenzi ili kukanusha tendo fulani. Mofu ya ukanushi ambayo huambikwa kwenye mzizi wa kitenzi cha Kinandi ni {ma-}. Kwa mfano:

(44) a. *Ma-a-kas* (sikusikia)
Kns-kptK-Mzz

b. *Ma-i-kas* (hukusikia)
Kns-kptK-Mzz

c. Ma-kas (hakusikia)
Kns-Mzz




**Kielelezo 17**.

Mifano zaidi ya ukanushi katika Kinandi ni kama ifuatayo:

(45)

| | **Kinandi** | | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| a. | Matieni | - | siimbi |
| b. | *Makitieni* | - | hatuimbi |
| c. | Metieni | - | huimbi |
| d. | *Motieni* | - | hamuimbi |
| e. | *Matien*i | - | haimbi |
| f. | *Matiendos* | - | hawaimbi |

Kibainishi cha ukanushi hubadilika kulingana na idadi na nafsi. Mofu inayotumiwa katika nafsi ya kwanza na ya tatu umoja ama wingi ya ukanushi ni {ma-}. Kwa upande mwingine, katika nafsi ya pili mofu hii hubadilika na kuwa {me-} katika umoja na {mo-} katika wingi.

## 17. HITIMISHO

Makala hii imechunguza mofosintaksia ya Kinandi na vipashio amilifu vimehakikishwa kwa kuvichomoza katika vielelezo tungo.

Katika uchambuzi huu, imebainika kuwa katika mofosintaksia ya Kinandi, kipatanishi kiima ni cha lazima na huchomozwa katika kielelezo tungo katika sehemu ya kiuamilifu ya kptK[1] na ni cha hiari. Isitoshe, kipatanishi kiima hutokea katika sehemu mbili: mwanzoni mwa kitenzi katika wakati uliopita na baada ya mzizi wa kitenzi katika wakati ujao. Kwa upande mwingine, kipatanishi yambwa hutokea mwishoni mwa kitenzi.

Mofu (-ki), (-ko) na (-ka) katika Kinandi ni tata kwa sababu zinabeba maana ya KptK na kibainishi cha wakati. Mofu za hali timilifu katika Kinandi ni {ko-}, {ke-} na {ka-}.

Kibainishi cha ukanushi hubadilika kutegemea idadi na nafsi. Katika nafsi ya kwanza na ya tatu umoja au wingi, mofu inayosimamia ukanushi ni {ma-} na katika nafsi ya pili umoja, ni {me-}. Isitoshe, mofu inayosimamia nafsi ya pili wingi ni {me-} pia.

Zaidi, imebainika kuwa tabia za vipatanishi kiima si dhabiti kwa sababu kibainishi chake hubadili nafasi au sehemu kinapokaa kulingana na muktadha au mada ya matumizi.

## 18. MAPENDEKEZO

Kulingana na matokeo ya utafiti huu inapendekezwa kuwa utafiti zaidi ufanywe ili kubainisha sehemu dhabiti ya kibainishi kiima katika kitenzi cha Kinandi. Ni wakati gani kielelezo kinachomoza kipatanishi kiima na njeo kwanza? Pia kibainishi {ki-) katika lugha ya Kinandi kichunguzwe zaidi kwa sababu ya utata

wake katika matumizi. Wakati mwingine kibainishi (ki-) hujitokeza kama kibainishi cha wakati na wakati mwingine kama nafsi. Hivyo, matumizi yake mengine yachunguzwe. Katika mofolojia ya Kinandi, sehemu ya kiima hubainishwe ili sehemu dhabiti ujulikane: Wakati mwingine hutokea kabla ya kibainishi cha wakati na wakati mwingine kabla. Aidha, nadharia ya kipekee inayochunguza lugha za Kitenzi - Kiima - Yambwa (TKY) ubuniwe.

## MAREJELEO


Chomsky, N. 1995.
*The Minimalist Program.* 'A Minimalist Program for linguistic theory'. Cambridge MA MIT Press. 28: 167–2170.

2000 *Minimalist Inquiries: The Framework.*Katika Step by Step: Essay in Minimalist Syntax in Honor of Howard Lasnik. Martin Micheals and Uriagereka (Whr). Cambridge, Mass, MIT Press 89–155.

Comrie, B. 1976.
*Aspect* 3–25 Cambridge: Cambridge University Press.

Creider, A.2002.
*The Semantics of Participant Types in Derived Verbs in Nandi.* http://id.erudit.org/revue/rql/2002/v31/n2/009316ar.pdf. Accessed 4/12/08.

Dal, O. 1985.
*Tense and Aspect Systems*. Oxford: Basil Blackwell.

Givón, T. 2001.
*Syntax.* Volume I. John Benjamins Publishing Co.

Hollis A.C 1909.
*The Nandi: Their Language and Folklore*. Oxford: Clarendon Press.

Lyons, J. 1995.
*Language and Linguistic: An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

Palmer, F. 1986.
*Mood and Modality.* Cambridge: Cambridge University Press.

TaaitaToweet (1979).
*A study of Kallenjin Linguistics*. Kenya Literature Bureau: Nairobi.


**About the author**: *Hellen Chesang' Barno* has a Master of Arts degree in the field of Kiswahili (Linguistics) and is an Assistant Lecturer in the Department of Languages in the School of Humanities and Social Sciences at the University of Eastern Africa-Baraton, P.O. Box 2500-30100, Eldoret-Kenya. She has admission to study for her PhD from Moi University Kenya and her area of interest is Kalenjin languages dynamics.